# MAELEKEZO YA KUTOA TAARIFA YA UPOTEVU WA MALI KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE LOSS REPORT)

**https://lormis.tpf.go.tz**

Hii ni tovuti kwa ajili ya kutoa taarifa ya upotevu wa mali yoyote kwa njia ya mtandao (**Online Loss Report**)

Ili uweze kufungua tovuti hii inakupasa uwe na sikanu (**smart phone)** au tarakilishi (**computer)** yenye mtandao. Fungua kivinjari (**Browser**) ulichonacho kwenye simu yako au tarakilishi yako, kisha andika tovuti hiyo kwenye kivinjari chako.

Mfano:




Baada ya kuandika tovuti kwenye kivinjari chako matokeo yake yatakuwa kama ifuatavyo;



## A) SAJILI MALI ILIYOPOTEA

Kwa mteja/mwananchi anayetoa taarifa kwa mara ya kwanza atabonyeza kitufe kilicho andikwa **sajili mali iliyopotea**.




Baada ya kubofya kitufe hicho utakuja ukurasa wa kujisajili.

Mteja/mwananchi anatakiwa asajili taarifa zake binafsi kwa usahihi kisha unabofya kitufe kilicho andikwa **hifadhi na endelea**



**ANGALIZO**

Hakikisha unakumbuka namba ya aina ya kitambulisho ulichochagua kujaza kwani hiyo namba ndio nywila **(password)** yako wakati wa kuangalia taarifa yako.

Baada ya kubofya kitufe cha **hifadhi na endelea** utapelekwa kwenye ukurasa ambao utaweza kutoa taarifa ya mali yako iliyopotea.

Baada ya kujaza taarifa zote kwa usahihi, bonyeza tena kitufe kilicho andikwa **hifadhi na endelea**.



Baada ya kubofya kitufe kilicho andikwa ‘*hifadhi na endelea*’ utapelekwa kwenye ukurasa ambao utakupatia au utakuonesha nambari ya malipo (**Control Number**) na namna malipo yanavyo weza kufanyika.




**ANGALIZO**

Malipo ya Taarifa ya Upotevu wa Mali (**LOSS REPORT**) ni **Tsh 500/= tu**.

1. Baada ya kulipia, tembelea kituo chochote cha **Polisi** kilicho karibu yako kwa ajili ya kuthibitishiwa taarifa ya upotevu wa mali yako.
2. Unaweza pata taarifa yako ya Upotevu wa Mali hapo hapo ulipo kama umetumia kitambulisho cha taifa (NIDA) na ikiwa umepoteza mali zifuatazo;- Laini ya simu,kitambulisho cha aina yoyote ile na kadi ya benki ya aina yoyote. Anagalizo hakikisha unachagua laini ya si,kitambulisho,kadi ya benki.
3. Pia, baada ya kuthibitishwa, unatakiwa kurudi kwenye tovuti ya **Kuripoti Mali Iliyopotea (https://lormis.tpf.go.tz)** kwa ajili ya kupakua (**Download**) taarifa yako.

Maelekezo ya kupata taarifa yako yapo kwenye kipengele namba **C** hapo chini.

Kama umepoteza mali zaidi ya moja haina haja kuanza upya kujisajili. Bofya maneno yanayosomeka **Ongeza mali iliyopotea.** Utapata ujumbe wa kukukumbusha kuhifadhi nambari yako ya malipo ya mali ya awali.




Katika dirisha litakalojitokeza likikutaka kuthibitisha kama unataka kuongeza taarifa ya mali nyingine iliyopotea;

- Bofya kitufe kilichoandikwa **NDIYO** utapelekwa moja kwa moja kwenye ukurasa wa kutoa taarifa ya mali yako iliyopotea badala ya kukupeleka kwenye ukurasa wa kuanza kuingiza taarifa zako binafsi.
- Hakikisha unahifadhi pembeni namba ya malipo ya taarifa ya kwanza kabla ya kubonyeza NDIYO kwani kwa kila mali unayoripoti kupotea utapewa nambari mpya ya malipo na inalipiwa Tsh. 500/-
- Tunza namba ya malipo kwa kila taarifa ya mali iliyopotea utakayoitoa kwa ajili ya malipo

- Bofya kitufe kilichoandikwa **HAPANA** kubakia hapohapo kwenye ukurasa wa maelekezo ya malipo ya taarifa yako ya kwanza ya mali iliyopotea.

## B) MTUMIAJI ALIYESAJILIWA TU

Kwa mteja ambaye tayari alishawahi toa taarifa kwa njia ya mtandao hana haja tena ya kuanza kujisajili upya bali ataenda kubofya kitufe kilicho andikwa **Mtumiaji aliyesajiliwa tu.**




Baada ya kubofya kitufe kilichoandikwa **Mtumiaji aliyesajiliwa tu** matokeo yake yatakuwa kama yafuatavyo kwenye picha. Hakikisha unayakumbuka majina yako matatu uliyojisajilia awali ili uweze kuthibitishwa.




Baada kubofya kitufe kilichoandikwa **thibitisha** utapelekwa kwenye ukurasa ambao utatoa taarifa ya mali yako iliyopotea.



Baada ya kubofya kitufe kilichoandikwa **hifadhi na endelea** utapelekwa kwenye ukurasa ambao utakupatia au utakuonesha nambari ya malipo (**Control Number**) na namna malipo yanavyoweza kufanyika.



## C) MAELEKEZO YA KUANGALIA TAARIFA YA MALI ILIYOPOTEA

Bofya kitufe kilicho andikwa **Angalia Taarifa yako**.




Baada ya kubofya kitufe kilicho andikwa angalia taarifa yako utaona ukurasa huu;




Hakikisha unajaza nambari ya malipo (Control Number) iliyo sahihi na nambari ya kitambulisho ulicho jaza wakati wa kujisajili. Baada ya hapo bofya kitufe chenye **alama ya kutafuta**.




Baada ya kubofya kitufe chenye alama ya kutafuta (3) utaletewa taarifa zako kama ifuatavyo;




Baada ya hapo bonyeza neno pakua ripoti (download) ili kupata taarifa yako kwa ajili ya kuinakilisha katika karatasi.



Baada ya kubofya kitufe cha kupakua utapata taarifa yako yenye muonekano kama huu hapa chini.



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
TANZANIA POLICE FORCE

LOSS REPORT

DAR/PHQ/RB/18419/2019

*This is to certify that*

AMANI GILLEAD TENGA

Reported to the police on **10 ,Machi 2019** that the under-mentioned property has been lost:-

| Property Type | Property Name | Property Number |
|---|---|---|
| Documents(eg.School,Car Card) | CHETI CHA KAZI CHA TFDA | - |

**More Details**

Nilikuwa nahama kutoka ofisi moja kwenda ofisi nyingine hivyo katika harakati za kuhama ndo cheti kile kikapotea.

**Control Number :: 991084852019**

INSPECTOR GENERAL OF POLICE (IGP)
16 ,Mei 2019

NB:It must be clearly understood that the certificate is not evidence that the report made by the complainants accepted by Police as genuine.